TANGAZO LA SERIKALI NA. 467 la tarehe 7/6/2024

# SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

## (SURA YA 290)

---

## SHERIA NDOGO

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale ambapo muktadha utaelekeza vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza;

"Jengo" maana yake ni nyumba au maendelezo yoyote yaliyofanyika kwenda juu au chini katika ardhi ndani ya Halmashauri;

"Kibali" maana yake ni ruhusa ya maandishi iliyotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Sura ya 290

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;

"ushuru" maana yake ni ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atalipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6. -(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1),

Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za usafirishaji wa bidhaa yoyote kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji wa madeni

7. -(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza mali hizo kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, itatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa

imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

8. -(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

10. -(1) Mtu yeyote anatenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa

kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atafanya biashara katika eneo la mamlaka ya Halmashauri bila kupata kibali.

Adhabu

11. Mtu atakayekiuka masharti ya kanuni yoyote katika Sheria Ndogo hii, atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani, atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa mujibu wa Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

| Namba. | Aina ya zao | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 JEDWALI LA KWANZA<br>*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*<br>SEHEMU A<br>USHURU WA MAZAO YA KILIMO | Pamba | Asilimia 3 ya bei ya soko |

*Tangazo La Serikalina. 467 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Alizeti | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 3 | Ufuta | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 4 | Choroko | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 5 | Tumbaku | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 6 | Dengu | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 7 | Kakao | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 8 | Mahindi | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 9 | Mtama | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 10 | Mpunga | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 11 | Karanga | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 12 | Mchele | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 13 | Kunde | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 14 | Ulezi | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 15 | Uwele | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 16 | Mbaazi | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 17 | Maharage | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 18 | Ndizi | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 19 | Kakao | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 20 | Fiwi | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 21 | Njugu Mawe | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 22 | Njegere | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 23 | Korosho | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 24 | Kahawa | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 25 | Mchikichi | Asilimia 3 ya bei ya soko ya mkungu |
| 26 | Mawese | Asilimia 3 ya bei ya soko ya ujazo wa lita 20 |
| 27 | Mise | Asilimia 3 ya bei ya soko ujazo wa debe |
| 28 | Matunda | 2,000/= kwa tenga moja |
| 29 | Tikiti maji | Asilimia 3 ya bei ya soko |
| 30 | Karoti au hoho au nyanya au vitunguu | 3,000/= kwa tenga moja |
| 31 | Mazao mengine ambayo hayajatajwa | Asilimia 3 ya bei ya soko |

SEHEMU B

USHURU WA MAZAO YALIYOCHAKATAWA

*Tangazo La Serikalina. 467 (Linaendelea)*

| Namba | Aina ya zao | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Unga (Kilo 25) | 250/= |
| 2. | Mafuta ya kupikia (lita 20) | 500/= |
| 3. | Mashudu (kilo 50) | 500/= |
| 4. | Chakula cha Mifugo (kilo 50) | 500/= |
| 5. | Pumba | 1,500/= |
| 6. | Mazao mengine ambayo hayajatajwa | 2,000/= kwa kilo 100 |

SEHEMU C

USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Namba | Aina ya zao | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya misitu | Asilimia 5 ya bei ya soko |

SEHEMU D:

USHURU WA MIFUGO MNADANI

| Namba | Aina ya mfugo | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 4,000/= |
| 2 | Ngamia | 4,000/= |
| 3 | Mbuzi | 1,500/= |
| 4 | Kondoo | 1,500/= |
| 5 | Nguruwe | 1,000/= |
| 6 | Punda | 1,000/= |
| 7 | Farasi | 1,000/= |
| 8 | Kuku | 500/= |
| 9 | Kanga | 500/= |
| 10 | Bata | 500/= |
| 11 | Wanyama wengine ambao hawajatajwa | 3,000/= |
| 12 | Aina nyingine ya ndege ambao hawajatajwa | 1,000/= |

SEHEMU E

USHURU WA KUSAFIRISHA MIFUGO

| Namba | Aina ya mfugo | Kiwango cha ushuru | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|---|

| | | (shilingi) ndani ya Wilaya | nje ya Wilaya |
|---|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 1,000/= | 1,500/= |
| 2 | Ngamia | 1,000/= | 1,500/= |
| 3 | Mbuzi | 500/= | 500/= |
| 4 | Kondoo | 500/= | 500/= |
| 5 | Nguruwe | 500/= | 500/= |
| 6 | Punda | 500/= | 500/= |
| 7 | Farasi | 500/= | 500/= |
| 8 | Kuku (kwa tenga moja) | 3,000/= | 3,000/= |
| 9 | Aina nyingine ya mnyama | 1,000/= | 1,500/= |
| 10 | Aina nyingine ya ndege | 2,000/= | 2,000/= |

## SEHEMU F

## USHURU WA HUDUMA ZA MIFUGO

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kuogesha ng'ombe | 500/= kwa ng'ombe moja |
| 2 | Kuogesha mbuzi | 300/= kwa mbuzi moja |
| 3 | Kuogesha kondoo | 300/= kwa kondoo moja |
| 4 | Kuogesha mbwa | 500/= kwa mbwa moja |
| 5 | Ngozi za ng'ombe | 150/= kwa ngozi moja |
| 6 | ngozi za mbuzi | 100/= kwa ngozi moja |
| 7 | ngozi za kondoo | 100/= kwa ngozi moja |
| 8 | ukaguzi wa nyama – ng'ombe | 3,000/= kwa ng'ombe |
| 9 | ukaguzi wa nyama – mbuzi au kondoo | 1,000/= kwa mbuzi au kondoo |
| 10 | ukaguzi wa nyama - nguruwe | 3,000/= kwa nguruwe |
| 11 | aina nyingine ya mfugo | 1,000/= kwa huduma |
| 12 | aina nyingine ya ndege | 500/= kwa huduma |

## SEHEMU G

## ADA YA LESENI NA USHURU WA SAMAKI

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Leseni ya uvuvi | Dola 10 |
| 2 | Leseni ya chombo cha uvuvi | Dola 10 |
| 3 | Leseni ya kukusanya samaki | Dola 4.56 |
| 4 | Samaki | 1,000= kwa kilo 50 |
| 5 | Dagaa | 1,000/= kwa kilo 50 |
| 6 | Samaki wa Mapambo | 500/= kila samaki |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Aina nyingine ya mazao ya majini | Asilimia 3 ya bei ya mauzo |

SEHEMU H

USHURU WA CHUMVI

| Namba | Aina ya Zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chumvi (out glowers) | 500/= kg 25 |

SEHEMU I

USHURU WA MAEGESHO

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) kwa siku |
|---|---|---|
| 1 | Teksi au bajaji | 500/= |
| 2 | Mabasi yanayofanya safari ndani ya wilaya<br>i. mabasi makubwa(ya abiria 26 na zaidi)<br>ii. mabasi ya kati/madogo( abiria 0-25) | <br>1,500/=<br>1,000/= |
| 3 | mabasi yanayofanya safari nje ya wilaya<br>i. mabasi makubwa(ya abiria 26 na zaidi)<br>ii. mabasi ya kati/madogo (abiria 0- 25) | <br>3,000/=<br>2,000/= |
| 4 | Pick – up au carry | 1,000/= |
| 5 | Trekta | 1,000/= |
| 6 | Lori chini ya tani 8 | 1,000/= |
| 7 | Lori kuanzia tani 8 hadi 12 | 2,000/= |
| 8 | Lori kuanzia tani 13 na kuendelea | 5,000/= |
| 9 | Magari madogo yanayofanya biashara ya kubeba abiria | 1,000/= |
| 10 | Mashine au mitambo ya ujenzi | 5,000/= |
| 11 | Maegesho maalum | 7,000/= |
| 12 | Magari binafsi | 500/= |
| 13 | Pikipiki za magurudumu mawili au matatu | 500/= |
| 14 | Baiskeli | 200/= |

SEHEMU J

USHURU WA KAZI ZA UTAMADUNI NA MICHEZO

*Tangazo La Serikalina. 467 (Linaendelea)*

| Namba | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha sherehe ukumbini | 30,000/= | Kwa kila sherehe |
| 2 | Ushuru wa waganga wa jadi au tiba asili | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Kibali cha kumbi za kuonyesha mpira na video:<br>(i) Maeneo yaliyopimwa<br>(ii) Maeneo yasiyopimwa | <br>30,000/=<br>10,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Kibali cha kuchezesha michezo ya bahati nasibu | 300,000/= kwa mashine | kwa mwaka |
| 5 | Kupiga muziki kwenye kumbi za starehe, baa na sehemu nyingine yeyote inayoruhusiwa | 50,000/= | kwa mwaka |
| 6 | Usajili wa vikundi au mtu binafsi au taasisi inayojishughulisha nashughuli za michezo au utamaduni na au sanaa | 40,000/= | kwa usajili |
| 7 | Kibali cha vikundi, mtu binafsi au taasisi inayoshughulika na shughuli za michezo, utamaduni na sanaa | 20,000/= | kwa mwaka |
| 8 | Kibali cha mashindano ya mpira au ligi au michezo mingine yoyote | 30,000/= | kwa ligi |
| 9 | Kibali cha kutumia uwanja wa Halmashauri kwa shughuli yoyote yenye kutoza kiingilio | 20,000/= | kwa siku |
| 10 | Kibali cha kutumia uwanja wa Halmashauri kwa mazoezi, mechi au shughuli yoyote isiyo ya kiingilio. | 10,000/= | kwa siku |
| 11 | Kibali cha msanii aliyetoka nje ya Wilaya kufanya tamasha | 50,000/= | Kwa kila tamasha |
| 12 | Kibali cha kufanya matangazo ya biashara katika maeneo ya wazi au barabarani | 30,000/= | kwa siku |
| 13 | Kibali cha usambazaji wa cable za luninga (tv) | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 14 | Kibali cha kuchezesha mchezo wa meza (pool table) au game na vinavyofanana na hivyo, kwa meza moja | 40,000/= | kwa mwaka |
| 15 | Kibali cha michezo ya sanaa za maonyesho yenye kiingilio yangoma au mziki au sinema au ngumi au mieleka au *kungfu* au mazingaombwe au sarakasi au maigizo | 20,000/= | kwa siku |
| 16 | Kibali cha michezo ya sanaa za maonyesho isiyo ya kiingilio ya ngoma au muziki au sinema au ngumi au mieleka au kungfu aumazingaombwe au sarakasi au maigizo | 10,000/= | kwa siku |
| 17 | Kibali cha kupiga muziki wa dansi (live band) au disko au tamasha | 30,000/= | Kwa siku |

*Tangazo La Serikalina. 467 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18 | Kibali cha kufanya shughuli za sanaa za ufundi kama uchoraji picha,upakaji rangi, uchongaji mihuri, vinyago na sanaa nyingine yoyote inayofanana na kundi hilo | 20,000/= | kwa mwaka |
| 19 | Kibali cha kunasa sauti au video au picha mnato wakati wa mashindano au shughuli iliyoandaliwa na Halmashauri | 10,000/= | kwa siku |
| 20 | Kibali cha uzinduzi wa album kwa wasanii wa ndani ya Wilaya | 20,000/= | kwa siku |
| 21 | Kibali cha kupiga muziki wa taarabu | 10,000/= | kwa Tukio |
| 22 | Kibali kwa mmiliki wa kumbi za burudani | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| 23 | Kibali cha kupiga picha za video | 10,000/= | kwa Tukio |
| 24 | Kibali cha mmiliki wa studio za kusafisha picha | 50,000/= | Kwa Mwaka |
| 25 | Kibali kwa mmiliki wa studio za kurekodi sauti | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 26 | Wamiliki wa studio za kurekodi filamu | 100,000/= | Kwa mwaka |
| 27 | Wamiliki wa majumba ya mazoezi(gym houses) | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 28 | Mabango yanayong'aa<br>i. Yenye ukubwa wa sqm 1 au chini ya hapo<br>ii. Yanayozidi sqm 1 ila hayazidi sqm 2<br>iii. Yanayozidi sqm 2<br>Yasiyong'aa<br>i. Yenye ukubwa wa sqm 1 au chini ya hapo<br>ii. Yanayozidi sqm 1 ila hayazidi sqm 2<br>iii. Yanayozidi sqm 2 | 100,000/=<br>200,000/=<br>250,000/=<br>50,000/=<br>100,000/=<br>150,000/= | Kwa mwaka<br>Kwa mwaka<br>Kwa mwaka<br>Kwa mwaka<br>Kwa mwaka<br>Kwa mwaka |
| 29 | Kibali cha kufanya shughuli za matambiko | 10,000/= | Kwa tukio |

SEHEMU K

ADA YA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Mali | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mitambo mikubwa | Kwa mujibu wa mkataba |
| 2 | Lori la tani 7 hadi 10 bila mafuta | Kwa mujibu wa mkataba |
| 3 | Gari dogo bila mafuta | 50,000/= kwa siku moja |
| 4 | Trekta | 70,000/= kwa siku moja |
| 5 | Ukumbi wa mikutano:<br>i. Ukumbi mdogo<br>ii. Ukumbi mkubwa | Kwa tukio<br>200,000/= kwa siku moja<br>500,000/= kwa siku moja |
| 6 | Kiti<br>Meza | 300/=kwa kiti 1 kwa siku 1<br>300/=kwa meza 1 kwa siku 1 |
| 7 | Darubini au GPS | 50,000/= kwa siku moja |
| 8 | Kutumia maeneo ya wazi au | 10,000/=kwa siku |
| 9 | Shamba | 50,000/= kwa ekari moja kwa Msimu |
| 10 | Kibanda eneo la soko kuu la Lugufu:<br>i. kibanda eneo la mzunguuko wa ndani<br>ii. kibanda eneo la mzunguko wa nje | <br>20,000/= kwa mwezi<br>25,000/= kwa mwezi |
| 11 | Nyumba ya kuishi mtumishi wa Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 12 | Mali nyingine ambayo haikutajwa | Kwa mujibu wa mkataba |
| 13 | Chumba cha kupangisha eneo la Mialo<br>i. Chumba kidogo<br>ii. Chumba kikubwa | <br>50,000/=<br>100,000/= |
| 14 | kibanda eneo la mnada wa mifugo wa Uvinza<br>i. kibanda chabiashara<br>ii. meza ya mama au baba lishe<br>iii. choo chamnadani | <br>50,000/= kwa mwezi<br>3,000/= kwa kila siku ya mnada<br>30,000/= kwa mwezi |

*Tangazo La Serikalina. 467 (Linaendelea)*

SEHEMU L

ADA YA ARDHI

**I.** HUDUMA ZA ARDHI

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya kiwanja cha ujenzi | 5,000/= kwa kila kiwanja |
| 2 | Ukaguzi wa mchoro wa ujenzi | 30,000/= kwa kila mchoro |
| 3 | Maombi ya hati miliki halisi | 5,000/= |
| 4 | Utafiti wa kitaalamu (official search) | 30,000/= kwa kila utafiti |
| 5 | Kuhamisha umiliki | 30,000/= kwa kila kiwanja kimoja |
| 6 | Kuoneshwa mipaka (plot identification) | 30,000/= kwa kila kiwanja au Shamba |
| 7 | Kkurudishia kigingi cha mpaka (beacon replacement) kufufua mipaka | 5,000/= kwa kila kigingi |
| 8 | Upimaji wa shamba | 50,000/= kwa ekari |
| 9 | Ada ya upimaji viwanja | 300,000/= kwa kiwanja |

**II.** KUBADILI MATUMIZI YA ARDHI

| Namba | AINA YA MATUMIZI | KIWANGO CHA ADA (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1 | Ombi la kubadili matumizi | 20,000/= |
| 2 | Nyumba ya makazi na biashara | 20,000/= |
| 3 | Nyumba ya biashara | 50,000/= |
| 4 | Nyumba ya kuishi | 10,000/= |
| 5 | Ghorofa<br>Ghorofa moja hadi mbili<br>Kwa kila ghorofa inayoongezeka | <br>200,000/=<br>100,000/= |
| 6 | Kiwanda au bohari au ghala. | 100,000/= |
| 7 | kubadili matumizi ya ardhi (makazi) | 50,000/= |
| 8 | kubadili matumizi ya ardhi (biashara) | 100,000/= |
| 9 | Kubadili matumizi ya ardhi (makazi na biashara) | 100,000/= |

**III.** ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| Namba | Aina ya ujenzi | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa mnara wa mawasiliano | 500,000/= kwa mnara |
| 2 | Ujenzi wa nyumba ya biashara | 100,000/= kwa nyumba |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Ujenzi wa nyumba ya makazi na biashara | 50,000/= kwa jengo moja |
| 4 | Ujenzi wa nyumba za makazi | 30,000/= kwa jengo moja |
| 5 | Ujenzi wa ghala au karakana au gereji au bohari | 200,000/= |
| 6 | Ujenzi wa kituo cha mafuta | 500,000/=kwa kituo kimoja |
| 7 | Ujenzi wa kiwanda kidogo au mashine za kukoboa na au kusaga nafaka | 200,000/= |
| 8 | Ujenzi wa ghorofa moja | 120,000/= |
| | Kwa kila ghorofa linaloongezeka | 80,000/= |
| 9 | Ujenzi wa chuo binafsi | 1,000,000/= |
| 10 | Ujenzi wa kiwanda | 2,000,000/= |
| 11 | Ujenzi wa shule | 500,000/= |
| 12 | kuweka uzio wakati wa kujenga jengo | 50,000/= |
| 13 | Ujenzi wa kibanda cha biashara | 10,000/= |
| 14 | Ujenzi wa jengo ambalo halijatajwa | Asilimia 3% ya gharama za ujenzi |

SEHEMU M

ADA YA VIBALI MBALIMBALI

| Namba | Aina ya shughuli | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ngoma za utamaduni | 10,000/= kwa siku |
| 2 | Maonyesho ( exhibition) [ya ndani ya nchi] | 5,000/= kwa banda kwa siku |
| 3 | Maonyesho ( exhibition) [ya kimataifa] | 500,000/= tukio zima. |
| 4 | Kununua pamba au tumbaku | 200,000/= kwa msimu |
| 5 | Kibali cha kununua mazao mchanganyiko | 50,000/= kwa msimu |
| 6 | Kufunga barabara kwa ajili ya sherehe | 20,000/= |
| 7 | Kibali cha kukata barabara ili kupitisha bomba | 30,000/= |
| 8 | Uuzaji wa dawa za asili na tiba mbadala | 40,000/= |
| 9 | Uuzaji vyombo vya majumbani | 20,000/= |
| 10 | Bonanza | 50,000/= |
| 11 | Ushuru wa choo | 300/= |
| 12 | Vyuma chakavu kwa tani | 5,000/= |
| 13 | Kitambulisho cha dalali mnadani | 40,000/= |
| 14 | Ukaguzi nyumba ya kulala wageni | 20,000/= |

SEHEMU N

ADA YA ZABUNI

| Namba | Aina ya zabuni | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Zabuni ya ujenzi wa majengo | 100,000/= kwa zabuni |
| 2 | Zabuni ya uwakala mbalimbali | 30,000/= kwa zabuni |
| 3 | Zabuni ya ugavi wa huduma | 70,000/= kwa zabuni |
| 4 | "Force account" | Asilimia 0.03% ya gharama ya zabuni |

SEHEMU O

USHURU WA SOKO, MNADA NA GULIO

| Namba. | Aina ya eneo | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Soko la lugufu (eneo la meza moja au kizimba au tandiko) | 6,000/= kwa mwezi au 200/= kwa siku |
| 2 | Masoko mengine (eneo la meza moja au kizimba au tandiko) | 9,000/= kwa mwezi au 300/= kwa siku |
| 3 | Soko au gulio - kuku | 500/= kwa kuku mmoja |
| 4 | Soko au manada au gulio-gunia la nafaka kilo 100 | 2,000/= |
| 4 | Mnada au gulio - kiwanja kimoja chabiashara au tandiko au kizimba | 10,000/= kwa mwaka |
| 5 | Mnada au gulio - baba au mama lishe | 500/= kwa mnada au gulio |
| 6 | Maeneo yote - kupakia mifugo katika lori – ng'ombe | 10,000/= kwa lori |
| 7 | Maeneo yote - kupakia mifugo katika lori– mbuzi au kondoo | 5,000/= kwa lori |

SEHEMU P

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya madini | Kiwango cha ushuru (shilingi) kwa meta mojaya ujazo |
|---|---|---|
| 1 | Mchanga | 1,500/= |
| 2 | Mawe | 1,500/= |
| 3 | Kifusi | 1,500/= |
| 4 | Kokoto | 1,500/= |
| 5 | Molalisi | 1,500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Udongo | 1,500/= |
| 7 | Aina nyingine ya madini ambayo haijatajwa | 1,500/= |

SEHEMU Q

USHURU WA NYUMBA YA KULALA WAGENI

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba ya kulala wageni | Asilimia kumi |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi………….. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ……………ya Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ya Mwaka, 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: …………………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Uvinza uliofanyika tarehe 18 mwezi Disemba Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

ACLAND DOMINIC KAMBILI
*Mkugenzi Mtendaji /Mkurugenzi wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza*

JACKSON FREDRICK MATESO
*Meya/Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Uvinza*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*